**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**April, 2024**

**Mbeya**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu:**

**Mkuu wa Shule-0786983912**

**Mwandamizi Taaluma-0757536055**

**Shule ya Sekondari Dr Tulia Ackson.**

**S.L.P. 1941,**

**MBEYA JIJI**

**Tarehe ....................…………….**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**…………………………………………….. S.L.P**
**……………………………………...**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI DR TULIA ACKSON HALMASHAURI YA MBEYA JIJI MKOA WA MBEYA MWAKA 2023/2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao...........................................amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Dr Tulia Ackson ipo umbali wa Kilometa 10 mashariki toka makao makuu ya mkoa (stand kuu.) Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi. Nauli ni Shilingi 700 na utashuka njia panda nzovwe na utapanda bajaji kwa kiasi cha shilingi 800.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ………………… hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ………………… Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………….

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia: -

### 2.1 SARE YA SHULE A. WAVULANA

i. Suruali mbili za rangi ya kijani 1 na rangi ya blue 1 za heshima siyo modo
ii. Mashati mawili yenye mikono mirefu aina ya tetron. Mashati yote ni lazima yawe marefu yawezayokuchomekewa ndani ya suruali, mfuko mmoja usio na mfuniko uje nayo.
iii. Jozi (pair) mbili za viatu vyeusi vya ngozi vya kamba. Visiwe na visigino virefu "ghorofa" au soli nene kupitakiasi. Viwe viatu vya kawaida vya heshima visiwe vya ajabu. Aidha huruhusiwi kuvaa raba au buti.
iv. Soksi za rangi nyeusi uje nazo na mkanda mweusi wa kawaida
v. Masweta mawili ya rangi ya **kijani cheusi (dark blue) yenye "V-SHAPE"** sehemu ya shingo uje nayo
**vi.** Raba nyeupe jozi moja na nguo za michezo ( **Track suit ya rangi ya blue** iliyokolea yenye **michirizimieupe pembeni)**
**vii.** Tai mbili za rangi **kijani**
**viii.** Mahitaji binafsi(nguo za ndani, sabuni, mswaki, mto na dawa ya memo ya kuswaki)

### B. WASICHANA

i. Mashati mawili meupe aina ya tetron mikono mirefu yawe marefu kuweza kuchomekea
ii. Jozi mbili za viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu au "ghorofa" au soli nene kupitakiasi pia zisiwe raba.
iii. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili au zaidi.
iv. Masweta mawili ya rangi ya kijani iliyokolea yenye **"V-SHAPE"** sehemu ya shingo uje nayo.
v. Sketi mbili za rangi kijani jeshi 1 na rangi ya **blue 1** zenye urefu wa kutosha nchi mbili kutoka kwenyeviatu (**Sketi zishonwe kwa Mtindo wa Rinda box**)
vi. Tai mbili za rangi **kijani** na **blue**
vii. Raba nyeupe jozi moja na nguo za michezo **( Track suit ya rangi ya blue iliyokolea** yenye **michirizi mieupe pembeni / ubavuni)**
viii. Rangi ya hijabu (kijuba)ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama**.**

**NB: Uniform kijani itavaliwa siku ya Jumatatu na Jumanne, Rangi ya blue itavaliwa sikuya Jumatano na Alhamis NA Track Suit itavaliwa siku ya Ijumaa kwa ajili ya michezo.**

### 2.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: -

i. Madaftari 8 (*quire 3*); na madaftari madogo aina ya msomi 8 kwaajili ya mazoezi.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mhula;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
vii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
viii. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mopa 1, mifagio 2 wa ndani na nje.
ix. Spring fail moja kwa ajili ya kuhifadhi nyaraka za mwanafunzi.

x. Fedha ya mahitaji ya mtihani wa utamilifu (mock) 20,000/= (italipwa akifika kidato cha sita. xi. Bima ya afya CHF 5000/= Mwenye kadi ya bima aje nayo na mchango huu hauta mhusu.

## 2.2 Michango mbalimbali

**a) Shule za Kutwa**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

**NB: Michango yote iliyopo kwenye jedwali (husika ilipwe kwenye akaunti ya shule : A/C NO. 61010070906 NMB** Jina la Akaunti **SHULE YA SEKONDARI DR TULIA ACKSON**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni Pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ✞ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ✞ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ✞ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

### 3.3 ORODHA YA VITABU MUHIMU KWA KILA SOMO

Unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu kulingana na masomo anayosoma. Orodha ya vitabu vinavyotakiwa kwa kila idara ni kama ifuatavyo;-

| **GENERAL STUDIES** | **ENGLISH** |
|---|---|
| 1. General studies for Advanced level certificate, form six (6) by Richard R.F Mbalase (2011)<br>2. General Studies for Advanced level certificate, form five (5) by Richard R. F Mbalase (2011)<br>3. Contemporary approach for Advanced level (General Studies Notes" Form five (5) and Form six (6) by Nyambari C. M Nyangwine, Steven O. Maluka (New syllabus 2009) | 1. Macmillan Education Ltd 2000, Encounters from Africa, Macmillan<br>2. Ayi Kwei Amah, 1996, The Beautiful Ones Are Not Yet Born, EAEP<br>3. Chinua Achebe, 1991, A Man Of The People, BAEP<br>4. Ndunguru 1999, Divine Providence, Mkuki Na Nyota.<br>5. Magala Nyago, 1985, the Rape of the Pearl.<br>6. Namige Kayondo, 1985 Vanishing |

**HISTORY**

1. Major issues in African History in Tanzania Institute of Education
2. History of Modern Europe by Peacock
3. How Europe Underdeveloped Africa by W. Rodney
4. History in Focus: Modern World History by Ben Walsh
5. Mastering Advanced level History book Two, by Kato, A (2011)
6. Mastering Advanced level History Book One by Kato, A (2021)

**GEOGRAPHY**

1. Principle of Physical Geography by Monkhouse (2008)
2. Landforms in Africa by Collin Buckle
3. Statistics Simplified by N. A Saleem
4. Map Reading by Mac Master
5. Human and Economics Geography by C. Morgan (1982)
6. Map Reading, General Publications Ltd – DSM by Durra, S. E. (2003)
7. Geography an Integrated Approach: Fouth edition by David Waugh (2009)
8. Practical Geography for Africa by John M. Pritchard (1990)
9. R. B. Bunnet (2007) General Geography in Diagrams

Shadows, Macmillan.

7. Danny Sato, 1983, His Excellency the Head of State, Macmillan.
8. David Ommowale, 2002, A Season Of Walting, EAEP
9. Francis Lubuga, 1990, Betray in The City, Heinnemann
10. Ngugi Wa Thiong'o, et al 1982, I Will Marry When I Want, EAEP
11. Bukenya, 1984, The Bride, EAEP
12. Okot Omitah 1991, Lwanda Megere Heinemann
13. Henrick Ibsen, 1974, An Enemy of The People, Eyre Matheuen
14. John Ruganda 2005, Black Mamba, EAEP
15. Charles Mloka, 2002, the Wonderful Surgeon and Other Poems, Mkuki Na Nyota.
16. Tanzania Institute of Education, 1996, Selected Poems, Print Pak (T) Limited.
17. The Real English Textbook Advanced Level, Dr. Kadeghe Michael.

**KISWAHILI**

1. Kimbunga - H. Gora (Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili) (TUKI), 1994
2. Mapenzi Bora – S. Robert (Mkuki na Nyota)
3. Chungu Tamu – T.A. Mvungi (Tanzania Publishing House), 1985
4. Fungate ya Uhuru – M.S. Khatibu (MacMillan and Aidan)
5. Vuta N'kuvute – Shafi (Mkuki na Nyota 1999)
6. Kufikirika – S. Robert (Mkuki na Nyota 2003)
7. Mfadhiliwa – Hussein Tawa (Methew & Stationery 2007)

| | |
|---|---|
| | 8. Usiku utakapokwisha – Mbunda Msokile 2007<br>9. Morani – E. Mbogo<br>10. Nguzo mama – P. Muhando<br>11. Kivuli kinaishi –<br>12. Kwenye ukingo wa Thim – E. Hussein<br>13. Kunga za Fasihi na Lugha – M. Msokile (1992)<br>14. Fasihi – F.E.M.K. Senkolo 1984<br>15. Kitangulizi cha tafsiri nadharia na mbinu – Mwansoko, H.J.M. (1996)<br>16. Nadharia ya Lugha kidato cha tano na sita – Suluhaya, M.C. (2 |

## 3.4 FOMU YA KUKUBALI

1. Mimi……………………………………. msichana / mvulana, ninakubali kuingia kidato cha ………………………………... shule ya Sekondari DR TULIA ACKSON kama mwanafunzi wa kutwa tarehe …………………... nitafika shuleni bila kuchelewa.
2. Nitatii sheria za shule na nitaishi kwa amani. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea
3. Sitashiriki katika Migomo, Fujo na makosa ya jinai.
4. Saini ya Mwanafunzi………………………………………Tarehe………………………………….

## SEHEMU YA MZAZI / MLEZI

1. Mimi …………………………………ninakubali mtoto wangu………………………….

   Asome katika shule ya Sekondari DR TULIA ACKSON kuanzia tarehe …………………………………
2. Ninaahidi kulipa Michango na pia kumpatia vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shuleni kama ilivyotajwa katika Barua na Fomu ya kujiunga na shule.
3. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi za kujitegemea
4. Ninakubali kuwa mtoto wangu amekubaliwa kuingia katika shule ya Sekondari DR TULIA ACKSON kama mwanafunzi wa kutwa.
5. Anuani yangu ya kudumu ni……………………………. Simu na………………………….
6. Saini …………………………………Tarehe ………………………………

3.**5** **FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**

**SHULE YA SEKONDARI DR TULIA ACKSON**

DR TULIA ACKSON SECONDARY SCHOOL,

P.O BOX 1941,

MBYEYA

………………………

…….. TO MEDICAL OFFICER……………………………

…………………………………………..

**PART A**

Mr. / Miss …………………………………………………………………………………………… …………….

Please examine the above-named student as to his / her physical and mental fitness for a full-time student in this school. The examination should include the following categories

1. Haemoglobin ………………………………………………………………………………………
2. P. V. Bleeding ………………………………………………………………………………………
3. Sight ………………………………………………………………………………………
4. Blood pressure ……………………………………………………………………………………
5. Urine for Sugar ………………………………………………………………………………………
6. Stool for routine examination …………………………………………………………………………………...
7. Pregnancy test ………………………………………………………………………………………
8. Skin diseases ………………………………………………………………………………………

9. Leprosy
…………………………………………………………………………………………
10. Any deformity
…………………………………………………………………………………………
11. Epilepsy
…………………………………………………………………………………………
12. Pulmonary tuberculosis
…………………………………………………………………………………...…
13. Neurosis
…………………………………………………………………………………………
14. Venereal diseases…………………………………………………………………………………
15. Other diseases
…………………………………………………………………………………………

### 3.6 TAARIFA BINAFSI (IJAZWE KIKAMILIFU NA IRUDISHWE SHULENI)

1. Jina lako kamili kama lilivyotumika kidato cha nne…………………………………….

   Dini yako/Dhehebu…………………………………………………………………

2. Jina kamili la baba mzazi/mlezi: ………………………………………………………...

   Kazi yake……………………………………………………………………………

   Anwani kamili ya baba mzazi/mlezi …………………………………………………….

   Na. yake ya simu ya mkononi…………… Na. yake ya simu ya mezani…………………...

   Mahali anakoishi baba mzazi/mlezi:

   Mkoa…………Wilaya……………..Tarafa……………… Kijiji/Mtaa……………………

3. Jina kamili mama mzazi/mlezi……………………………Kazi yake………………………

   Anwani kamili ya mama mzazi/mlezi………………………………………………….

   Na. yake ya simu ya mkononi……………. Na. yake ya simu ya mezani …………………

   Mahali anakoishi mama mzazi/mlezi: Mkoa………………… wilaya…………….

   Tarafa…………………………………. Kijiji/Mtaa……………………………...

4. **Majina ya watu watano wanaoruhusiwa kumchukua mtoto wako baada ya kuitwa na uongozi wa shule. (kumbuka hakuna siku ya kuwatembelea wanafunzi)**

| Na | Jina lake | Uhusiano | Mahali anakoishi | Anwani na namba yake ya simu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |

.

5. **Shule nilizosoma msingi hadi kidato cha nne**

| Na | Jina la shule | Darasa/Kidato | Kuanzia mwaka hadi mwaka | Mkoa | Wilaya | Kijiji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | | |
| 2. | | | | | | |
| 3. | | | | | | |
| 4. | | | | | | |

Namba yangu ya mtihani wa kidato cha nne………………...

6. **Matokeo yangu ya mtihani wa kidato cha nne.**

| Na | Somo | Daraja |
|---|---|---|
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |

Nilipata divisheni…………………... Pointi……………...

7. Tarehe niliyoripoti hapa Iduda Sekondari ni ………………………... Masomo nitakayosoma ni:
   1. ……………………………. ……… 2. ……………………………………...
   3. ………………………………… 4. ……………………………………….
   5. …………………………………………
   6. ………………………………...
8. Matarajio yangu baada ya kumaliza kidato cha sita ni:
   1. ………………………………………………………………………………………..
   2. ………………………………………………………………………………………..
   3. ……………………………………………………………………………………….
   4. ………………………………………………………………………………………
9. Hapa shuleni ningependa nijiunge na:
   1. Michezo: (i) ………………………... (ii) ……………………… (iii) ………………………...
   2. Kikundi cha utamaduni wa…………………………………………………………..

Mradi wa……………………………………………………………………

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**
    i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
    ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
    iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
    iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule.…………………………………….**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………...**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0786 983 912**
- **Mwandamizi Taaluma 0757 536 055**